**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

## TAARIFA KWA UMMA

## MAMLAKA KUFANYA TATHMINI YA WATOA HUDUMA YA UFUKIZAJI NCHINI KWA MUJIBU WA SHERIA YA AFYA YA MIMEA

**07 Januari, 2026 Arusha**

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) imeundwa kwa Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Namba 4 ya 2020, Sura Na. 133 (Plant Health Act. No. 4; Cap. 133) kwa lengo la kuweka mfumo wa pamoja wa kisheria wa usimamizi na udhibiti wa afya ya mimea na mazao ya mimea ili kukidhi matakwa ya masoko ya mazao na mikataba ya kimataifa ikiwemo International Plant Protection Convention (IPPC). Aidha, Mamlaka pia imekasimiwa kusimamia na kudhibiti matumizi ya viuatilifu ili kuweka mazingira salama kwa afya ya binadamu, Wanyama na Mimea.

TPHPA inapenda kuutaarifu Umma kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea Na. 4 ya Mwaka 2020 na Kanuni za Afya ya Mimea za mwaka 2023 na mabadiliko yake ya 2024 inakusudia kufanya tathimini kwa Watoa Huduma ya Ufukizaji (Fumigation Service Providers) wa mazao ya kilimo, Meli za shehena za mazao, mbao na maghala ya kuhifadhi nafaka nchini kuanzia tarehe 14 Januari hadi 29 Januri, 2026 ili kujiridhisha kuwa huduma hiyo inatolewa kwa mujibu wa matakwa na viwango kama vilivyoainishwa na Sheria na Kifungu cha 34 cha Kanuni za Afya ya Mimea.

Hivyo basi, Watoa Huduma ya Ufukizaji mnaaswa kutoa ushirikiano kwa Watumishi wa Mamlaka watakaofika katika Ofisi au eneo lako la kazi ili kuwezesha zoezi hili kufanyika kwa ufanisi. Mtoa huduma yeyote ambaye hatahakikiwa na TPHPA hatoruhusiwa kuendelea kutoa huduma husika mpaka atakapohakikiwa.

Aidha, Mamlaka itaanza kupokea maombi ya Wadau wapya wenye nia ya kuomba kufanya shughuli za ufukiziaji baada ya zoezi hili kukamilika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu kupitia registrar@tphpa.go.tz; simu namba +255-684 560877 au +255713-364963.

Imetolewa na,

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY
ARUSHA - TANZANIA

Prof. Joseph C. Ndunguru
**MKURUGENZI MKUU**